

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA TISA

01 JUNI, 2017



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA TISA – TAREHE 01 JUNI, 2017

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Nishati na Madini juu ya Makadirio

ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**317. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY
(MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Serikali ina mpango gani wa kuwalipa posho au mishahara Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ili kurahisisha ufanisi wa shughuli zao.

**318. MHESHIMIWA JUMA SELEMANI NKAMIA
(CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wilaya ya Chemba haina Hospitali jambo linalowalazimu Wananchi wake zaidi ya laki tatu kwenda kupata huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Kondoia:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuhakikisha Wilaya hiyo inapata Hospitali.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

**319. MHESHIMIWA SAUMU HERI SAKALA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kando kando mwa Bahari ya Hindi Mkoani Tanga pameibuka bandari bubu ambazo nyingine zinakuwa kubwa na kuhudumia watu wengi zaidi na Askari wasio waaminifu hufanya bandari bubu hizo kuwa vyanzo vyao vya mapato kwa kuchukua rushwa kwa watu wanaopitisha mizigo yao katika bandari hizo:-

Je, ni lini Serikali itazirasimisha bandari hizo na kuzifanya zitambulike ili Wafanyabiashara wanaozitumia wawe huru.

**320. MHESHIMIWA BALOZI DKT. DIODORUS
BUBERWA KAMALA (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Serikali iliunda Bodi ya Kusajili Wakandarasi (CRB) ambayo ina jukumu

la kusajili, kuratibu na kusimamia mwenendo wa Makandarasi nchini:-

(a) Je, tangu kuanzishwa kwa CRB ni Wakandarasi wangapi Watanzania wamesajiliwa na Taasisi hiyo;

(b) Je, Serikali Kuu na Halmashauri za Wilaya zinatumia vigezo gani kutoa kazi kwa Wakandarasi.

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

321. MHESHIMIWA DEVOTHA MATHEW MINJA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:- Mchango wa kazi za Wasanii umeonekana katika kutoa ajira lakini bado Wasanii wanakabiliwa na changamoto mbalimbali za kuhujumiwa kazi zao ambapo Mheshimiwa Rais ametoa maagizo mbalimbali ya kushughulikia watu wanaohujumu kazi za Wasanii:-

Je, mpaka sasa ni hatua gani zimechukuliwa.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**DODOMA
01 JUNI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**

